TOLEO NO.69

# Khilafah

NDIO SULUHISHO

JUMADA THANI 1447 HIJIRIA — DESEMBA 2025 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

## MAASKOFU NA MASHEIKH MSIKUBALI KUTUMIKA VIBAYA MKASABABISHA MAAFA





Tanzania inaendelea kutafunwa na mgogoro wa kisiasa tangu siku ya uchaguzi 29 Oktoba 2025 na baada. Mgogoro huo umepelekea vifo, uharibifu wa mali za Umma, za serikali, binafsi pia miundombinu.

Katika hali ya kushangaza na kusikitisha pamoja na kuwa mgogoro huo unahusu siasa za kidemokrasia lakini tumeshuhudia hata baadhi ya viongozi wa kidini wakijitosa ndani yake, hali inayotishia taharuki zaidi ya kijamii.

Kiini cha migogoro ya siasa inayochipuka katika nchi changa kama Tanzania na nchi zote ulimwengu wa tatu kuna mahusiano moja kwa na mfumo thakili wa kibepari unaotawala leo dunia.


Nchi zote change leo zipo chini ya mikono ya mabepari wa Marekani au Ulaya ambao ndio wamiliki wa mfumo huo wa kibepari.

Mfumo ambao kipimo chao katika matendo ni maslahi tu, hata iwe ni kwa kuyafuata maslahi hayo juu ya mafuvu ya vichwa vya watu.

Na ili kufikia maslahi hayo wakoloni mabepari hutumia njia na mbinu yoyote iwe halali

**Inaendelea Uk. 3**

## WAZAZI NA MALEZI KIPINDI CHA LIKIZO YA WANAFUNZI



Mwezi wa Disemba ya kila mwaka huwa ni muda wa likizo ndefu ya mwisho wa mwaka kwa shule za msingi na sekondari. Ni kipindi ambacho wanafunzi hupata fursa adhimu ya muda mrefu wa mapumziko kando na harakati zao za kimasomo za miezi mingine.

Kipindi hiki ni muhimu kwa wazazi na walezi kuwapa watoto wao muongozo na mwelekeo maalumu kwa ajili ya kuwajenga na kuwafinyanga kwa mustakbali mwema kifamilia na jamii kwa jumla.

Jambo nyeti wanalopaswa kufahamu wazazi na walezi ni kwamba elimu ni mchakato endelevu kwa mtoto au kwa mwanadamu kwa jumla. Na kwa kuwa wao ni sehemu ya walimu wa watoto hao, basi hawana budi kukitumia kipindi hiki cha likizo kuendelea

**Inaendelea Uk. 7**

### Yaliyomo :


- **Tupambane na tatizo msingi la ubepari na sio matawi yake…....2**
- **Kushiriki maziko ya kafiri……………………………………………………4**

# TUPAMBANE NA TATIZO MSINGI LA UBEPARI NA SIO MATAWI YAKE

Tanzania imekumbwa na mgogoro wa kisiasa tangu siku ya uchaguzi 29 Oktoba 2025 na baada kwa masiku kadhaa, hali iliyopelekea vifo na uharibifu wa mali na miundombinu.

Kama ambavyo tunasema mara zote kwamba demokrasia ambayo ni nidhamu ya kisiasa ya kibepari pamoja na utaratibu wake wa vyama vingi ililetwa na wamagharibi wakoloni kwa maslahi yao wenyewe, si kwa matakwa, maslahi wala maendeleo ya nchi zetu kama inavyodhaniwa na wengi, kiasi cha baadhi ya watu kuchanganyikiwa kwa matumaini hewa, wakipoteza muda mwingi, rasilmali na hata kupoteza maisha kwa kutarajia mabadiliko.

Mfumo huu wa demokrasia ya vyama vingi ulileta na wakoloni kwa hila na udanganyifu ili kuwabadilishiabadilishia watu sura ya mtawala. Kwa sababu (wakoloni) waligundua kwamba watu wamechoshwa na kulikuwa na kiasi kikubwa cha malalamiko kutokana na ukatili wa mfumo wa chama kimoja uliotetwa na kulindwa na hao hao (wamagharibi) baada ya kutupatia uhuru bandia wa bendera. Kwa mfumo huo wamagharibi pia wanalenga huwahadaa wananchi kwamba na wao wana nafasi ya maamuzi, jambo ambalo si kweli, hata Marekani raia hawachagui raisi wao kwa njia ya moja kwa moja.

Kwa hivyo, sera hii ya vyama vingi ililetwa kama mbinu nyingine ya kuupa nguvu ukoloni mamboleo baada ya ukoloni mkongwe na uhuru bandia (wa bendera) ili kuwaondosha watu kufikiri kwa usahihi dhidi ya mfumo mzima wa kibepari. Ikawa sasa, badala ya watu kupambana kung'oa mfumo muovu wa kibepari uliotamalaki na kunyonya ulimwenguni kote hususan nchi changa, watu wakabaki wanatumia nguvu zao zote katika suluhisho la uwongo la kubadilishabadilisha sura za watawala ilhali tatizo msingi ambalo ni mfumo wa kibepari lipo pale pale.

Bila ya kusahau kuwa, uchaguzi huo (wa vyama vingi) pia ni mkakati wa wakoloni wa kurefusha uhai wa mfumo wao wa kibepari na wakavifanya vyama pinzani viwe silaha ya akiba dhidi ya watawala wa ulimwengu wa tatu. Pale vyama tawala wasipolinda vyema maslahi ya wakoloni, basi vyama pinzani vitapewa nguvu ya kumtoa madarakani mtawala. Lakini mtawala akilinda maslahi yao vizuri vyama pinzani vitaendelea kubakia kama watazamaji tu.

Pia ni wazi kwamba nchi za kikoloni za magharibi wamekua wakitumia sera ya vyama vingi na visingizio vyengine kuchochea mizozo kwa raia, migawanyiko na vurugu ili kwa ujanja kufanikisha kwa urahisi unyonyaji wao wa rasilimali za (nchi changa). Mifano hai ni kama: Sudan, Kongo, Yemen, Somalia nk.
Kwa bahati mbaya kuna wanaodhani kwamba demokrasia ya vyama vingi ndio huleta maendeleo ilhali kuna nchi nyingi changa zinazotekeleza demokrasia ya vyama vingi, ilhali rasilmali zao zinahodhiwa na mataifa ya magharibi, raia wao bado wanahangaika katika hali duni ya umaskini na nchi zao bado zimebaki kuwa watumwa wa mataifa ya magharibi.

Kwa kumalizia, kila mmoja afahamu kuwa tatizo kubwa na msingi duniania leo ni mfumo mzima wa kibepari ambao umetamalaki kila mahala duniani ukipewa nguvu na kusimamiwa na mataifa makubwa, na kamwe kubadilisha sura ya mtawala hakubadilishi chochote zaidi ya kujichosha na kupoteza rasilmali.

Suluhisho la kweli sio kuwa na mfumo wa vyama vingi, bali ni kuung'oa mfumo mzima wa ubepari katika uso wa ardhi na kuweka mfumo mwengine mbadala wa haki na uadilifu ambao sio mwengine bali ni Uislamu chini ya kivuli cha dola yake ya Khilafah Rashidah

**Mhariri**

**Jumada thani 1447 Hijria**

**Desemba 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

*******************

## Maaskofu na Masheikh ... *Kutoka uk .1*

au haramu. Aidha, kwa misingi ya kibepari uchaguzi sio njia pekee ya mtawala kupata madaraka. Tunaona nchini Saudia na sehemu nyengine zenye ufalme, mtawala anarithi kiti ilhali hata bila ya uchaguzi, ilhali Marekani na Ulaya wanamtambua. Aidha, tunaona nchi kama Misri mtawala Al-Sisi alimpindua mshidi halali wa kidemokrasia, hata hivyo Al-Sisi ni kipenzi mkubwa wa madola ya kibepari.

Kwa hivyo, sio kweli kwamba wamagharibi wapo kujali uchaguzi, haki za binadamu na demokrasia. Bali wapo kuangalia nani atalinda maslahi yao.

Kwa upande mwengine, wamagharibi huutumia uchaguzi kama mbinu tu ya kurefusha uhai wa mfumo wao wa kibepari kwa kuwahadaa wananchi kwamba na wao wana nafasi ya kufanya maamuzi, jambo ambalo si kweli, hata Marekani raia hawamchagui raisi wao kwa njia ya moja kwa moja kwa maamuzi ya moja kwa moja ya raia. Kwa hivyo, ni dhahiri uchaguzi sio njia pekee ya kumfikisha mtawala madarakani.

Ikumbukwe pia wakoloni wameandaa mfumo wa vyama vingi ili vyama pinzani viwe kitisho kwa watawala wa ulimwengu wa tatu, kwamba lau watawala hao waliopo madarakani wasipolinda vyema maslahi ya wakoloni, basi vyama pinzani vitapewa nguvu ya kumtoa mtawala madarakani. Lakini mtawala huyo huyo lau atalinda vyema maslahi ya wamagharibi wakoloni, vyama pinzani vitaendelea kubakia kuwa wapenzi watazamaji. Kimsingi, wakoloni huongozwa na kanuni kwamba wao hawana rafiki wala adui wa kudumu, bali wana maslahi ya kudumu.

Vyama pinzani ni kama vyama tawala hawana suluhisho mbadala. Na vyama vyote (tawala na upinzani) hunyenyekea mabwana wao wa magharibi na mfumo huo huo wa kikoloni wa kibepari, mfumo katili na thaqili kwa viumbe.

Hivyo, wapinzani wakinadi kufuatwe demokrasia maana yake na wao ni watumishi wa mfumo huo wa mabepari kama watawala. Wote wanakimbilia kutafuta suluhisho kwa mabepari ambao ndio hao hao waliyoingamiza Iraq, Afghanistan, Libya, Yemen, Sudan, Kongo nk. ambapo mabepari sio tu wanapora mali, bali katika maeneo mengine kama Kongo na Sudan wanamaliza pia roho za raia wanyonge kupitia magenge yao yenye silaha. Basi iweje makatili kama hawa wawe na huruma kwa raia wanyonge wa nchi za ulimwengu wa tatu?

Mabepari katika kufikia wepesi wa kunyonya rasilmali za nchi changa hutumia mbinu ya kuwadhoofisha wanajamii kwa kupitia mbinu na migogoro kadhaa wa kadhaa, kama vile vyama vya siasa, ukabila, umajimbo, udini, urangi bali hata umadhehebu kwa watu wa dini moja ili kuwasha moto wa ugomvi na chokochoko.

Leo kwa masikitiko makubwa baadhi ya masheikh na maaskofu wana shambuliana kutetea siasa chafu za kiuwongo za kidemokrasia, lakini kesho wanasiasa wakiuunganishwa na kuletwa pamoja na mabepari kwa kugawana mkate, masheikh na maaskofu hao hao watalazimika kula matapishi yao, utawaona kwa fedheha wanarudi kulingania umoja baina ya wananchi. Bali wanaweza hata kwenda mbali zaidi hadi kulingania wito wa kimakosa wa 'dini mseto' (ukuruba baina ya dini)

Ukweli ni kuwa hakuna mwanasiasa yoyote wa kidemokrasia awe dini yoyote atakayokuwa anaingia madarakani kwa maslahi na malengo ya dini, bali atawatumia watu wa dini kwa kipinidi tu cha kuwahitajia. Kwa kuwa mfumo anaoutumikia wa kidemokrasia hauna dini.

**Nasaha kwa Masheikh,**

Tunawambia baadhi ya masheikh wanaojitosa katika migogoro ya wanasiasa wa kidemokrasia chonde chonde, nyinyi mna mfumo bora na safi wa Uislamu ambao una muongozo wa kila kitu, basi msikubali kutumika na wanasiasa. Hata kama tunakiri kwamba upande wa pili kuna athari ya ubaguzi wa kidini kihistoria, lakini tofautisheni baina ya taasisi ambazo ndio hutenda na kubeba ajenda ubaguzi huo wa kidini na sio wakiristo binafsi. Pia tambueni kuna wakiristo wengi wasiokuwa madhehebu ya kikatoliki. Bali kubwa zaidi fikra za kibaguzi wa kidini zilizopo Tanzania zinazobebwa na taasisi za kikatoliki chimbuko lake ni mfumo wa ubepari na ukoloni ili kuleta na kukuza fitna za kijamii.

Basi simameni kupambana na

**Inaendelea Uk. 6**

## KUSHIRIKI MAZIKO YA KAFIRI

**Swali:**
Hukmu ya muislamu kushiriki ibada ya kumzika ndugu yake kafiri, na Mtume (SAAW) alifanyaje wakati wa kumzika ami yake?

**Jibu:**

Inajuzu kwa muislamu kushiriki katika kumzika kafiri katika jamaa zake wa karibu, kwa yale yaliopokelewa na Abu Daud na wengineo, toka kwa Ally (RA) amesema : ***"Nilimwambia Mtume (SAAW): Hakika ami yako ni mtu mzima aliyepotea na amekufa, akaniambia "Nenda kamfukie Baba yako, kisha usiongee chochote mpaka uje kwangu" Nikaenda kumfukia na nikaja kwake. Mtume (SAAW) akaniamrisha nikaoge na akaniombea dua"*** Hadithi hii iko wazi kwamba Mtume (SAAW) alimuamrisha Ally akamzike baba yake Abi Twalib na yeye alikuwa ni mshirikina, ikaonyesha kuruhusiwa kufanya hivyo …

Hii ikiwa kuzika ni kwenye mchanga, ama ikiwa si katika mchanga basi si ruhusa kwa muislamu kushiriki katika jambo hilo, kwa sababu Allah amesema :

{ مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَى}

**"Kutokana na udongo tumekuumbeni, na ndani ya udongo tutakurudisheni, na kutokana na huo udongo tutakutoeni kwa**



**mara nyingine."**
Ama ikiwa si katika yale yalioelezwa na uislamu, kama vile kuchomwa moto, basi hairuhusiwi kwa muislamu kushiriki katika ibada hizo za maziko.

Ama kuhusu alifanyaje Mtume (SAAW) wakati wa maziko ya Ami yake, ni kwamba yeye Mtume (SAAW) hakushiriki katika maziko yake na alimtaka Ally akamzike baba yake, na pamoja kwamba Mtume (SAAW) hakushiriki katika maziko, lakini alimuamrisha Ally akamzike Baba yake, hii inaonyesha kuruhusiwa kwa jambo hilo.

Na jambo muhimu kulitaja hapa ni kuwa hukmu ya kushiriki katika ibada za kimazishi za makafiri kama vile swala za maiti na mfano wa hayo, haifai kushiriki katika ibada hizo kwa maiti wa makafiri kwa namna yoyote ya ukaribu uliopo, nayo ni kwa sababu *"La Ilaaha Illa-Llah"* ambayo ndio alama ya uislamu ina maana ya kwamba hakuna ambaye anastahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah; na kwamba swala na ibada za makafiri kwa maiti wao ni katika mambo ya kiibada yalio kinyume na *"La Ilaaha Illa-Llah"* kwa hiyo haifai kwa muislamu kushiriki katika swala zao za maiti au kushiriki katika maombi na misa zao kwa namna yoyote ilio ya ukaribu wao.

Na pia kuna namna nyingine katika mas-ala haya kama vile kuosha muislamu maiti ya jamaa yake kafiri na kufuata jeneza lake, mimi nakunukulia rai za wana Fiq-hi katika mas-ala haya mawili kwa ajili ya kupata faida .

**1 – Kushiriki katika kuosha maiti wa makafiri**

Wamekubaliana wana Fiq-hi kuwa si wajibu kwa muislamu kumuosha kafiri… Ama upande wa kujuzu kulifanya hilo wametofautiana wana Fiq-hi wa Madhehebu, wapo walioruhusu na wapo waliozuia…. Na nakunakilia rai zao ili ufuate katika mas-ala haya rai ya madhehebu ambayo utakinaika nayo :

A - Kwa Mahanafi : Ikiwa maiti ya kafiri ana ndugu zake wa karibu waislamu, na wala hakuna wa kulifanya hilo katika watu wa dini yake na mila yake, basi ni ruhusa kwa ndugu zake waislamu kumuosha, kama wapo wa dini yake basi muislamu atawaachia wao wamuoshe.

B - Madhehebu ya Shafii: Ni ruhusa kwa waislamu na kwa wengineo kuwaosha makafiri; na ndugu zake makafiri

**Inaendelea uk..5**

wenziwe wana haki zaidi kuliko ndugu zake waislamu.

C - Madhehebu ya Maliki na Hambali : Muislamu hamuoshi kafiri hata kidogo, sawa ni ndugu yake wa karibu au si ndugu yake wa karibu.

**2 – Kushiriki Kusindikiza Maiti wao baada ya kukamilisha Ibada zao:**

A – Mahanafi : Imepokelewa kwao kwa upande wa muislamu kwenda kusindikiza jeneza la ndugu yake kafiri au jamaa yake wa karibu kwamba inaruhusiwa, lakini awe mbali na asiwe karibu nao …, na hayo yamekuja kwenye kitabu "Durarul Hukaami Fii Sharhi Ghuraril Ahkaam", mtunzi wake ni Muhammad Bin Faraamirzi Bin Ally, mashuhuri kwa jina la Mula Khasru aliekufa Mwaka 885 Hijria (…. Na afuate Jeneza kwa Mbali, hii kwa yule ambaye ukafiri wake si wa Kuritadi …..)

B – Kwa Maliki: Asibebe muislamu jeneza la kafiri na wala asilisindikize na wala asimzike… katika kitabu "Annawadiru Wazziyaadaat Alaa Maa Fiil Mudawwanah Min Ghairihaa Minal Ummahaat" Kilichotungwa na Abdallah Bin AbdirRahmaani Alqairawaaniy Almaalikiy Aliyefariki 386 Hijria yamekuja haya yafuatayo: "Amesema Ibn Rajabu: Asibebe Muislamu Jeneza la Kafiri na wala asilisindikize na wala asimzike….

Na hata kama Muislamu atafiwa na Jamaa yake kafiri kama vile baba, mama, kaka nk, basi hakuna ubaya wa kushiriki na kusimamia jambo lake na atajiweka mbali na watu wa dini yake, kama watatosheleza na kukawa na usalama wa kutokupotea atawaacha wamzike, na kama ataogopea hilo basi awe mbele yao kwenye kaburi lake na kama hakuogepea kupotea kwake na akapenda kuhudhuria maziko basi awe mbele ya jeneza lake huku akijitenga nalo na wale wanaolibeba. Imepokelewa kwa Mtume (SAAW) kuwa ameruhusu hivyo. Amesema Atwaa: Na yule ambae mama yake Mnaswara akafariki, ana haki ya kumkafini na kusimamia maziko yake na akasindikiza jeneza huku akijitenga na mambo yao. Amesema Ibn Rajab: Kupanda na kutembea vyote ni sawa sawa katika hilo. Amesema Malik: Hakuna ubaya kusimamia msiba wake wote kisha awakabidhi watu wa dini yake, na wala asifuate jeneza isipokuwa akichelea kupotea, basi atachungulia kwenye kaburi lake na wala asiingie humo isipokuwa itakapokuwa hakuna wa kulifanya hilo.

C – Kwa Mashafii : Inajuzu kwao kufuata jamaa wake wa karibu kafiri… Imekuja kwenye kitabu "Almajmuu Sharhel Muhadhab" cha Mtunzi Zakariyyah Muhyid diin Yahya Bin Sharafu Annawawi aliekufa mwaka 676 Hijria" (Amesema Imam Shafii katika kitabu kiitwacho *Mukhtasar Almuzany* na wafuasi wake kuwa inajuzu kwa muislamu kufuata jeneza la jamaa yake wa karibu alie kafiri…)

D – Kwa Mahanbali: Inajuzu kwa Muislamu kufuata jeneza la mzazi wake kafiri, lakini iwe mbele ya jeneza na wala sio nyuma yake… Imekuja katika Mughni ya Ibn Quddaamah Almaqdisy aliyekufa mwaka 620 Hijria, amesema Ahmad (kuhusu Myahudi au Mnaswara aliekufa na ana mtoto Muislamu, na apande kipando na aende mbele ya Jeneza…)

Ndugu yenu Ata bin Khalil Abu Rashta

*******

## BAADHI YA MATUKIO MWEZI JAMADUL- AKHIIR

**1. Mtume SAAW kuanza kulelewa na kunyonyeshwa na Bi. Halima Al-Saadiya**

**2. Doria ya Zaid bin Harithah**

**Kikosi hiki cha askari 100 kilitumwa kuwadhoofisha makureish na kuandaa mazingira ya vita. Kilifanikiwa sana kuwatia hasara makureish na kuchangia kutokea vita vya Uhud (3AH Hijri)**

**3.Kutumwa kwa Kikosi eneo la A-taraf**

**Kikosi hiki kilitumwa ama A-taraf au Al- twaraq kikiwa chini wa uongozi wa Zaid bin Harithah na askari 15 kupambana na Bani Tha'alabah ambao walikimbia, waislamu wakapata ngawira ya ngamia 20 waliowawacha.(Mwaka wa 6AH)**

mfumo wa kibepari katika msingi wake, na fikra hizo za ubaguzi nazo zitaanguka, kwa kuwa hazina uwezo wa kusimama wenyewe. Nyinyi mna dini ya Uislamu yenye nguvu ya kifikra na mfumo huo umewapa thaqafa ya ujasiri wa kutosha.

Tambueni vuguvugu hili la kidemokrasia litapita. Basi chungeni sana msije mkasimama upande mchafu katika historia, mkaacha athari ya mapigano baina ya Waislamu na wakristo. Jambo hilo litawafanya siku ya Qiyama kubeba mzigo mkubwa. Basi Masheikh, maustadh na Waislamu kwa ikhlasi tunawaelezeni bebeni ajenda ya Uislamu na sio ajenda za kidemokrasia.

Aidha, tanabahini kuwa, Uislamu hauruhusu kuuwa mtu isipokuwa kwa sheria na vidhibiti maalumu. Vivo hivyo, haifai kuunga mkono mtu kuuliwa au kudhuriwa kwa kukosoa jambo ambalo halina uhusiano kamwe na Uislamu.

Fahamuni masheikh mnaojitosa katika wimbi hili yeyoye anayesimama upande wa wauaji, waporaji au waharibifu wa mali, atasimama nao siku ya Qiyama kwenye hesabu, akiwa miongoni mwao kwa kosa la kuua, kudhuru au kuharibu mali za watu au mali za Umma.

**Nasaha kwa Waislamu,**

Jihadharini misije mkachezewa akili kwa kutangaziwa jihadi feki. Jihadi ni kupigana kwa ajili ya Allah Taala kwa malengo ya kutanua Uislamu au kujilinda, na sio kutetea utaifa au wanasiasa wa kidemokrasia ambao hawahukumu kwa Uislamu, bali hata hawapo tayari kabisa kuutumikia Uislamu. Atakayeua au kuuliwa kwa kushiriki mapambano kama hayo ajue ana kesi ya kujibu siku ya Qiyama.

Enyi Waislamu, msije mkajazwa chuki dhidi ya wasiokuwa waislamu kwa maslahi ya wanasiasa, kwani Uislamu haufundishi chuki kwa asiyekuwa Muislamu madam hana vita dhidi ya Uislamu.

Ikumbukwe kwamba katika zama za dola ya Kiislamu wakristo na watu wengine wasiokuwa Waislamu waliishi kwa amani na wakishirikiana na Waislamu bega kwa bega katika Maisha yao, hata pale wakristo wenzao kutoka Ulaya walipovamia miji ya Kiislamu, wakristo hao wanaoishi katika miji ya Waislamu walishirikiana na Waislamu kupambana dhidi ya wakristo wenzao wa Ulaya.

Uislamu unachokataza ni kushirikiana na wakiristo na watu wa dini nyengine katika mambo ya kidini kama vile 'dini mseto' nk. Lakini haukatazi kuamiliana na wakiristo na wasiokuwa Waislamu katika miamala ya kiuchumi, kusaidiana, ujirani mwema nk.

Aidha, tunawaasa Waislamu, panapokua na mahasimu wa pande mbili sio lazima Muislamu kuunga mkono pande moja ya mgogoro huo, kwani imawezekana pande zote mbili hakuna inayoungwa mkono na Uislamu. Hivyo, tusichotwe na mihemko kutaka lazima tuunge mkono upande mmoja, kwani twaweza kutumbukia kwenye haramu.

Enyi Waislamu, hakikisheni sheria ndio inayoongoza katika kuunga mkono, kupinga, kujitenga na pande zote, na muingalie haki kwa mujibu wa Uislamu na sio kwa kipimo cha kidemokrasia au kwa matamanio ya nafsi.

**Nasaha kwa Maaskofu,**

Dini yenu haina siasa, kudandia kwenu kwenye siasa za kidemokrasia ni dalili nyongeza kwamba dini hii sio ile ya Nabi Issa As. Kwa masikitiko dini yenu ilikua wakala wa kurahisisha ukoloni, na mpaka leo imebakia kuwa wakala rasmi wa mabepari wakoloni. Na ndio maana tuhuma za kutumika kuleta vurugu na mauaji maeneo kadhaa duniani ni nyingi na zipo wazi. Mfano, Rwanda, Kongo nk.

Bila ya kusahau kanisa limekuwa likibeba ajenda nyingi za mabepari kama za 'dini mseto' ushoga, kuzuiya kuzaa kwa wingi, ndoa za wake wangi, ndoa za mapema mnazoziiita ndoa za utotoni nk.

Hivyo, madai yenu katika qadhia za kisiasa lazima yatiliwe mashaka sana kwani asili huwa yana msukumo nyuma ya pazia, imma msukumo wa wakoloni au maslahi yenu binafsi.

Hapa labda tuwaulize mnatumia kipimo gani cha kulaani mauaji na maafa ya wanaoitwa waandamanaji kama sio wanamapinduzi, lakini hamkulaani mauaji ya Kibiti, Mkuranga, Mtwara, Rufiji, Pemba nk.

Wanaoitwa waandamanji waliovamia mali za watu binafsi, mali za Umma na kuharibu miuondombinu ya Umma, inakuwaje muone jambo hilo ni jambo halali? Jee wanaodaiwa kuwa waandamanaji-

**Inaendelea Uk. 7**

mnaowaunga mkono walishindwa kuandamana (japo maandamano hayo hayatuhusu Kiislamu) bila kuharibu mali na kusababisha madhara? Tunaelewa wazi kwamba nafsi ya mtu ina thamani kuliko mali. Bali hilo sio kibali cha kuharibu mali, iwe mali ya mtu binafsi, mali ya Umma au mali ya serikali. Baya zaidi Maaskofu mlikuwa kimya wakati baadhi wakiwemo makasisi wa kikiristo walipokuwa wakihamasisha mapema juu ya uharibifu wa mali hizo na kuleta madhara hayo.

**Nasaha kwa Wanasiasa,**

Chukueni hadhari kutoka kwa hawa waitwao viongozi wa dini wenye kutuhumiwa 'uchawa' ambao wapo kulinda maslahi yao binafsi kwa kutumia tiketi ya dini kwa madai ya kudai haki na uadlifu ambao hurusha maneno yenye kuhimiza au kuashiria vurugu baina ya Waislamu na wakristo.

Lau mwenye nia mbaya wa ndani au nje, awe Muislamu au mkristo mwanasiasa au yeyote atafanya mashambulizi kwa kiongozi yeyote wa dini yoyote, kisha wafuasi wa dini hiyo wakataka kulipa kisasi kwa njia ya kiholela basi jambo hilo litasababisha machafuko ya wenyewe kwa wenyewe, ambayo ni machafuko mabaya katika jamii inayoishi pamoja.

Hivyo, viongozi wa dini wanaorusharusha maneno yenye ishara hizo wakatazwe mara moja, kwani wao hutoa maneno hayo kujipendekeza kwenu. Fitna ya ugomvi wa kidini ikiripuka kuizima itakuwa tabu na itapoteza roho za wengi wasio na hatia.

**Nasaha kwa wote,**

Tunaunasihi Umma wote kwa jumla Waislamu na wasio kuwa waislamu huu ni muda muafaka wa kuona kwamba mfumo huu wa kidemokrasia sio mfumo sahihi na salama kwa mwanadamu.

Dunia nzima inawaka moto kwa machafuko, vita, njaa, maradhi, mivutano ya kisiasa unyanyasaji kutokana na mfumo huu.

Basi kwa wasiokuwa Waislamu tunatoa kwenu mwito wa kurudisha akili zenu kuutafiti Uislamu kwa jicho la insafu na uadilifu, bila ya shaka na mtaukuta una nidhamu bora ya kiutawala na muafaka kwa ustawi bora wa mwanadamu hapa duniani na kesho akhera.

Amma kwa Waislamu washiriki katika wajibu wa ulinganizi wa Uislamu ili kurejesha mfumo wake wa utawala wa Khilafah, unaotarajiwa kurudi si muda mrefu, kwa kuanzia ardhi kubwa za ulimwengu wa Kiislamu na kuenea duniani kote ukitawanya kheri na uadilifu kwa Waislamu na kwa wanadamu wote bila ya ubaguzi wa rangi, jinsia wala dini.

**************

*Usikose Jarida lako la Khilafah Kila mwezi*






kuwapa watoto elimu, japo sio kwa sura ya elimu ya shule.

Kwa bahati mbaya baadhi ya wazazi huwaachia watoto wao huria katika muda kama huu kuwaruhusu kurandaranda na kuzurura mitaani bila ya mwelekeo thabiti au mpangilio wenye muongozo kwa sababu tu wamefunga shule. Jambo hili ni hatari kwa ustawi wa watoto hao na jamii kwa ujumla. Na kimsingi mtoto ukimuacha bila ya muongozo katika miamala yake, kuna uwezekano akakugharimu katika maisha yake.

Katika kipindi kama hiki wazazi hususan wa Kiislamu wanaweza kuchukua mwelekeo ufuatao kuwasaidia katika kuamiliana na watoto wao ambao wako likizo.

**1.Kufuatilia nyendo zao kwa umakini**

Japo ukweli unabaki kwamba mzazi na mlezi huwa ana jukumu wakati wote kufuatilia mwenendo wa mtoto wake, akiona mazuri ampongeze na kumuhimiza na akigundua mapungufu amrekebishe, lakini kipindi hiki ni fursa pana zaidi kwa wazazi na walezi, kwa kuwa fursa ya kuamiliana na mtoto inakuwa kubwa zaidi. Aidha, ni muhimu mzazi kufuatilia mwenendo wa mtoto katika upande wa kiibada kama swala, kuongeza maarifa ya thaqafa ya Kiislamu kama kusoma vitabu,

**Inaedelea uk 8**

kufanya ulinganizi, usomaji Quran nk. Japo asili haya ni mambo ya wakati wote lakini muda huu ni muda wa kupatiliza zaidi. Na kama mzazi atagundua mtoto hayuko vizuri humlazimu kufanya marekebisho.

**2. Kujadili maendeleo ya kimasomo**

Wazazi na walezi hupaswa kuketi kirafiki na watoto wao kujadili maendeleo ya masomo na changamoto mbalimbali zinazomkabili mtoto. Jambo hili mbali na kuwa na faida moja kwa moja katika upande wa kimasomo ya mwanafunzi, lakini pia lina maana pana zaidi ikiwemo kumjenga na kumfinyanga mtoto utamaduni wa kujifunza kutafiti tatizo, kulijadili na kutafuta suluhisho. Bila ya kutaja kukuza urafiki na kumtanua upeo wa mtoto kimawasiliano.

3. **Kurekebisha fahamu za kimakosa.**

Wazazi na walezi yawapasa wajue kwamba wakati wote wana jukumu la kusahihisha fahamu za kimakosa ambazo watoto hupewa katika elimu ya kisekula. Tukumbuke kwamba kwa kuwa elimu hii inatokana na hadhara/ mfumo wa kimagharibi wa kibepari ndani yake imeingizwa mafikra na manadharia mengi kinyume na Uislamu. Fikra kama binadamu kutokana na sokwe (evolution), usawa baina ya mume na mke, fikra ya dini mseto', fikra za kiuwongo kama za 'uhuru' haki za wanawake, haki za binadamu, fikra ya kuwa Uislamu hauna nidhamu ya kiutawala nk. Kimsingi fikra zote hizo ni batil na zinazotokamana na mfumo wa kidemokrasia na zinazogongana moja kwa moja na misingi ya Uislamu. Wazazi na walezi watakua na masulia/ dhima mbele ya Muumba baada ya kuwapeleka watoto katika mashule haya bila ya kuweka sawa fahamu hizo katika mabongo yao. Bali mbali na kuweka sawa fikra hizo, ni wajibu pia kuwashirikisha watoto katika amali ya ulinganizi wa Khilafah, kwa kuwa hiyo ndio silaha ya kupambana na fikra hizo. Ni vyema na wajibu wazazi kutumia vyema likizo hii kujiondoa katika dhima hiyo.

4. **Kuamilina nao katika mambo ya kifamilia na kijamii**

Katika muda huu wazazi na walezi pia hupaswa watenge muda wa kujumuika na watoto kwa kuketi pamoja, kuzungumza kirafiki, kujadili qadhia za kifamilia, kucheza, kula pamoja, kwenda msikitini, mazikoni, kusoma Quran pamoja, kufanya visomo vya dua na watoto wao ili kukuza mazingira ya ukuruba na mapenzi, na kuziepusha nyumba zetu kuwa kama kambi za kijeshi. Kwani hili ni haki yao na haki ya wazazi na walezi kwa watoto hawa, na pia baada ya likizo hawapati muda wa kuwa karibu zaidi na wazazi wao kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari ambapo mzazi hupelekwa mchakamchaka na kazi , na mtoto hushughulishwa na mzigo wa manadharia katika masomo yake.

5. **Kuwafundisha na kuwashirikisha katika stadi za maisha**

Huu ni muda ambao wazazi na walezi pia wautumie vyema kukuwafundisha watoto wao stadi za maisha. Kuwafundisha kazi kama kujenga, umeme, fundi bomba, kushona kuwashirikisha watoto kivitendo walau wawe na maarifa msingi ya kivitendo juu ya stadi hizo. Pia kuwaonesha majukumu yao, haki, wajibu wao kwa wazazi, ndugu, jamaa, majirani na marafiki nk.

**6. Kuwafundisha kujenga udugu**

Ni wajibu kuwafundisha watoto kujenga na kuimarisha mshikamano wa udugu. Nalo linaweza kutendwa kwa namna moja katika mbili. Amma kufanya ziara na watoto kwa ndugu na jamaa ili wajuane vyema. Amma wazazi au walezi wanaweza kuwaruhusu watoto kubakia kwa ndugu kwa kufanya ziara kama mazingira yanaruhusu japo kwa siku chache.

7. **Kuwapa muda wa mapumziko.**

Na mwisho, wazazi na walezi lazima wayatende mambo kwa uzani wa hali ya juu ili kuwapatia watoto muda wa kutosha wa mapumziko. Watoto hawa hushughulishwa na masomo muda wote wawapo shuleni, hivyo ni muhimu na wajibu kupata muda wa kupumzika zaidi. Hivyo, wazazi wasiwanyime watoto haki yao hii kama binadamu.